OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

SIMU: 0684 306666 / 0754034233 – mkuu wa shule
0759 442207 - makamu mkuu wa shule
e-mail:kisiwanisekondari@ yahoo.com

SHULE YA SEKONDARI
KISIWANI,
S.L.P. 31,
SAME.

Kumb Na.KSS/S735/OG/ 08 **Tarehe: 25/03/2022**

JINA LA MWANAFUNZI ……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KISIWANI JULY 2022, MICHEPUO YA HKL /HGK.

YAFUATAYO NI MASHARTI NA MAHITAJI MUHIMU:

A. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujinga na kidato cha tano katika mchepuo wa **HGK/HKL kwa** mwaka wa masomo 2022/2023 katika shule ya sekondari Kisiwani. Kwaniaba ya Bodi ya Shule, Waalimu, Wafanyakazi na Wanafunzi wa shule hii nakupa pongezi na kukukaribisha kwa moyo wa kindugu hapa shuleni.

Napenda kuchukua nafasi hii kukumbusha maneno ya Mheshimiwa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na yale yasemwayo serikalini kuhusu Elimu ya Sekondari “Kuchaguliwa kwako ni bahati na wala sio stahili (Haki) yako na kuwa una deni kwa nchi yako, Serikali na Wananchi”. Ukija hapa ni kama umetumwa na Wananchi walio vijijini uje uvune taaluma na kurudi kusaidia ukishavuna. **HILI NDILO LENGO LAKO UTAKAPOKUWA HAPA SHULENI.**

Ukiwa hapa shuleni utakuwa na wajibu mkubwa wa kusoma kwa bidii, kufuata sheria za shule na kushiriki katika shughuli za Ellimu ya kujitegemea. Shule itafunguliwa kwa mhula wa kwanza kwa kuzingatia maelekezo yatakayotolewa na Serikali.
Shule ya sekondari Kisiwani ipo **Wilaya ya Same**, Mkoa wa**Kilimanjaro**, Mashariki mwa barabara kuu ya Dar-es-Salaam – Arusha. Shule ipo umbali wa **kilometer 30** toka Same Mjini. Unapofika Same Mjini shuka kituo kikuu cha mabasi. Hapohapo uliza magari **yaendayo Kisiwani, Gonja na Ndungu**. Ukifika Kisiwani uliza mahali shule ilipo, ni umbali wa meta 300 kutoka kituo cha magari Kisiwani mjini.Kwa wanaotoka Dar es Salaam kuna Basi la moja kwa moja linalokuja hadi Kisiwani linaitwa SHETCO (Ukiwaeleza unashuka kisiwani sekondari watakushushia getini kabisa).

NB:Usitumie usafiri wa **pikipiki** kutoka SAME hadi **Kisiwani (nauli ya gari kutoka Same-Kisiwani ni 2,000/=)**

Utalazimika kufanya yafuatayo:

a) Naambatanisha Fomu ya Hospitali- FOMU A. itakupasa uende kupimwa afya yako na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya yako (District Medical Officer)**.** Fomu B & C zijazwe mbele ya mzazi na uje nazo shuleni.
b) Uje na vyeti halisi (original) na vivuli vyake kama ifuatavyo:
   - Result slip
   - Cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)
   - Cheti cha kuhitimu kidato cha Nne (leaving Certificate)
   - Passport size (02) yenye blue kwa nyuma na awe amevaa shati la shule.
   - Folder file mbili (02)-rangi ya khaki

MZAZI/ MLEZI MWANDALIE MWANAO MAHITAJI YAFUATAYO:

i. Godoro inchi $2^{1}/_{2}$ x 6'.
ii. Shuka mbili (02) rangi ya pink, mto, foronya na blanket moja (01)
iii. Sanduku la bati kwa usalama wa vifaa vyake.
iv. Taulo,sabuni, mswaki na dawa, rangi ya viatu.
v. Sahani, kijiko,bakuli na kikombe
vi. Chandarua kimoja (01)
vii. Kanda mbili jozi moja (01)

VIFAA VYA TAALUMA:

i. Daftari 06 (4 Quire) kalamu ya bluu au nyeusi, pensile na rula.
ii. Kofa / mkebe (mathematical instrument) kwa wanaosoma Jiografia.
iii. Scientific calculator kwa wanaosoma Jiografia
iv. Ream moja ya karatasi-A4 kwa mwaka kwa ajili ya majaribio ya kila wiki na mitihani mingine endelevu.
v. English Dictionary (kamusi ya Kiingereza) na vitabu vingine vya Kiingereza kwa wanaosoma Kiingereza
vi. Kamusi ya Kiswahili na vitabu vya Kiswahili (kwa wanaosoma Kiswahili)
vii. Vitabu vya Jiografia (kwa wale wanaosoma Jiografia)
viii. Vitabu vya Historia (kwa wale wanaosoma Historia)

MICHANGO YA SHULE:

NA	AINA YA MCHANGO	KIASI (TSH)
1	Ada kwa mwaka	70,000/=
2	Taaluma kwa mwaka	20,000/=
3	Kitambulisho	6,000/=
4	Nembo	3,000/=
5	Ukarabati	15,000/=
6	Wapishi,walinzi na vibarua wengine	30,000/=
7	Huduma ya kwanza na bima ya Afya	15,000/=
8	Mtihni wa Utamirifu (mock VI)	20,000/=
9	Tahadhari	5,000/=
	JUMLA	**184,000/=**

AKAUNTI ZA SHULE:

- MALIPO YOTE YAWE KWE KATIKA **AKAUNTI YA SHULE YA SEKONDARI KISIWANI NAMBA 40501100015 (NMB) -Kisiwani secondary school Education. Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi unapofanya malipo bank.**

Kisha ulete risiti (pay In slip) kutoka benki uliyolipia malipo hayo ya shule. HATUPOKEI FEDHA TASLIMU

SARE ZA SHULE:

- Shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi
- Suruali mbili (02) rangi ya khaki zisizobana -zenye marinda na mkunjo chini(Turn-up)
- Soksi jozi mbili (02) au zaidi- nyeupe
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi (sio raba)
- Sweta rangi ya khaki aje nalo (lenye "V" shingoni) – Makoti hayaruhusiwi
- Mkanda mweusi wa ngozi wa suruali. Mikanda yenye bakoli kubwa hairuhusiwi shuleni.
- Aje na suruali mbili nyeusi za **kitambaa** za heshima za **kushindia**(Suruali isiyo ya kitambaa mf. jeans hairuhusiwi)
- Aje na T-shirt mbili rangi ya blue yenye kola na isiwe na **maandishi yoyote** (isiwe light wala duckblue)

NB:Nguo za nyumbani haziruhusiwi isipokuwa sare ulizoelekezwa uje nazo hapo juu

VIFAA VYA MICHEZO:

- Raba jozi moja (01)
- Jezi (Bukta rangi ya nyekundu na T-shirt nyeupe-HGK), bukta bluu na t-shirt njano kwa HKL

VIFAA VYA USAFI:

- Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko .
- Soft broom (01) kwa HGK na Squeezer (01) kwa HKL
- Reki (HGK) na jembe na mpini wake (HKL) (01)

MAAGIZO MUHIMU:

- Kila mwanafunzi lazima asome sheria, kanuni na taratibu za shule kwa uangalifu, azifuate na kuzitii, kutokufanya hivyo ni kosa.
- Uvunjaji wa sheria za shule hata ikiwa ndogo kiasi gani hautavumiliwa
- **SIMU ZA MKONONI HAZIRUHUSIWI**
- Mzazi /Mlezi ampatie mwanae fedha ya matumizi (pocket Money)
- Mzazi / Mlezi atamgharamia mwanae nauli wakati wa kuja shuleni na kurudi nyumbani
- Mzazi / Mlezi atamgharamia mwanae anaporudishwa nyumbani kwa ajili ya kutofuata sheria, taratibu na kanuni za shule muda wowote atakapofanya kosa hilo.
- Mzazi /Mlezi atamgharamia mwanae bahasha na stamp kwa ajili ya kutuma matokeo kwa kila muhula. (Pia mzazi / mlezi alete anwani sahihi itakayotumika katika kutuma matokeo kwako)

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE:

.

SHERIA ZA JUMLA:

1. a) Yampasa kila mwanafunzi kumpa heshima mtu yeyote anayemzidi umri kwa (kusimama na kuamkia) wakati wowote.

   b) kila mwanafunzi lazima awe mtiifu kwa walimu wote, wafanyakazi wote, viranja wa shule na wakuu wengine wote. Ubishi au ujeuri wa aina yeyote kwa walimu au kiranja ni kosa kubwa.

2. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalimu bila ruhusa au sababu maalum. Maeneo waishio wafanyakazi wa shule ni nje ya mipaka ya wanafunzi.
3. Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na Mkuu wa shule tu kwa kushauriana na Mwalimu wa zamu, mlezi wa nyumba au mwalimu wa darasa pale itakapo lazimu
4. Wizi, uzinifu, ugomvi, matusi ni makosa makubwa haviruhusiwi.
5. Usafi binafsi (wa mwili na roho), mavazi, mabweni, viwanja vya shule ni muhimu kwa kila mwanafunzi.
6. Heshima na tabia njema shuleni na nje ya shule ni wajibu wa kila mwanafunzi.
7. Ni wajibu wa mwanafunzi kuheshimu, kuthamini, kupenda na kufanya kazi kwa uwezo wake wote
8. Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule, mali ya Jamii au Taifa. Ni kosa kuharibu au kutumia vibaya mali ya umma
9. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika barua kwa Mkuu yeyote bila kupitisha (U.F.S) kwa Mkuu wa shule
10. Kila mwanafunzi lazima afuate ratiba ya shule kikamilifu wakati wote
11. Kofia zozote, miwani nyeusi na nguo za ajabu zisizokuwa na maadili haziruhusiwi.
12. Mwanafunzi atanyoa nywele zake vizuri na zitabaki fupi. Vipara, pank na kufuga ndevu hairuhusiwi na haitavumilika
13. Wanafunzi wote watavaa sare za shule stahili wakati wote wawapo shuleni au wakirudi nyumbani wakati wa likizo na kuja shuleni.
14. Vikundi vyote vya Dini vitafuata taratibu za shule kwani shule haina dini.

SHERIA ZA MADARASA:

1. Mwanafunzi lazima kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa kwani kutega kipindi inahesabika kuwa ni kosa la utoro ambalo linaweza kumwondoa mwanafunzi shuleni
2. Hairuhusiwi kulala bwenini muda wa vipindi isipokuwa kwa kibali maalum tu.
3. Kelele za aina yeyote darasani haziruhusiwi, kwani darasani si mahali pa kupiga kelele.
4. Wakati wowote mwalimu akiingia darasani ni lazima wanafunzi wote wasimame kwa heshima na kumwamkia. Halafu mwalimu atatoa ruhusa ya kukaa.
5. Wanafunzi watahakikisha usafi na unadhifu wa darasa lao kila siku kabla ya masomo kuanza.
6. Mwanafunzi lazima afanye mazoezi na mitihani ya masomo yote yanayofundishwa darasani kwake. Ni kosa linaloweaza kumfukuzisha mwanafunzi shule kwa kuacha kufanya mazoezi/ mitihani bila sababu za msingi.

SHERIA ZA BWENI:

1. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchemsha / kupika kwa kutumia moto wa kuni, mkaa, mafuta ya taa au moto wa umeme
2. Ni marufuku mwanafunzi kupeleka chakula bwenini
3. Bwenini ni mahali pa kulala si pa kupiga kelele. Usemi wa Bweni uwe mazungumzo ya maana ya sauti ndogo. Upigaji wa kelele au mayowe ni dalili za ulevi, uhuni, fujo nk. Hivyo haikubaliki.
4. Usafi wa bweni ndani na nje (Mazingira yanayozunguka bweni) ni wajibu wa kila mkaaji wa bweni husika.
5. Ni makosa kukaribisha mgeni wa aina yoyote bwenini au katika eneo la bweni.
6. Vyoo vyote lazima vitumike vizuri na kuwekwa katika hali ya usafi
7. Ni wajibu wa viongozi wa bweni pamoja na wanabweni wote kulinda sheria kwa kuzitekeleza kwa vitendo.
8. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoroka usiku na wakati wa maandalizi ya masomo ya jioni (evening preparations)
9. Kuzima taa na kulala ni saa 4:00 usiku.
10. Ni kosa kumruhusu mtu wanje kuchota maji bwenini.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji, ulawiti na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji sigara, bangi, cocaine, mirungi, kuberi nk.
4. Makosa ya jinai
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kusababisha mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba /kushiriki kutoa mimba.
11. Kunyanyasa wanafunzi wenzake.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kudharau walimu na walezi
14. Kukataa adhabu kwa makusudi.
15. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KISIWANI.

_____

RICHARD A. MWETA
MKUU WA SHULE

FOMU A

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

SIMU: 0684 306666
0754 034233
e-mail:kisiwanisekondari@ yahoo.com

SHULE YA SEKONDARI KISIWANI,
S.L.P. 31,
SAME

Kumb Na.KSS/S735/MEF/F5/09 **Tarehe: 25/03/2022**

MGANGA MKUU,
……..
……..

YAH: **UCHUNGUZI WA AFYA YA MWANAFUNZI.**

Mwanafunzi …… amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika Shule ya sekondari Kisiwani. Kabla ya kujiunga katika shule hii na kuendelea na masomo ni lazima apimwe afya yake kama inamruhusu kuendelea na masomo ya kidato cha tano. Tunaomba umfanyie uchunguzi.(Medical examination).

NA.	MAGONJWA	NDIYO (V)	HAPANA (X)
01	Masikio		
02	Macho		
03	Kifafa		
04	Moyo (heart disease)		
05	Magonjwa ya akili (Mental illness)		
06	Ukosefu wa damu (Anemia sickle cells)		
07	Kifua kikuu (T.B)		
08	Pumu (Asthmatic case)		
09	Kisukari		
10	Vidonda vya tumbo		
11	Kichocho (Bilharzias)		
12	Magonjwa ya zinaa (sexual Transmitted Diseases)		

Je ana dosari nyingine kiafya/ Ugonjwa mwingine (Eleza)
……
……

MAELEZO YA DAKTARI: Baada ya uchunguzi. Nimeona/ sikuona dosari yoyote katika afya ya mwanafunzi huyu. Ametibiwa/ Hakutibiwa/ Hastahili/ Anastahili kuendelea na masomo (kata isiyohusika)
……
……

_____
MKUU WA SHULE
KISIWANI SEKONDARI

FOMU B

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

1. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi:…….
Tarehe ya kuzaliwa:…….
Uraia Mtanzania / Sio Mtanzania:……
Shule ya msingi aliyotoka:……...
Jina la mzazi/mlezi:…….
Anwani ya mzazi/mlezi:……
Kitongoji /kijiji anapoishi mzazi/mlezi:……..
Namba za simu za mzazi/mlezi:……...
Kazi ya mzazi / mlezi:……

2. MKATABA WA KUZINGATIA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Mimi ……..(jina la mwanafunzi) nakiri kuwa nimesoma na kuelewa maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Kisiwani. Naahidi kuzingatia na kwamba nikienda kinyume na maelekezo hayo niazibiwe na kufukuzwa shule itakapokuwa imelazimu.

Tarehe:………… **Sahihi:……**

FOMU C-MZAZI/MLEZI

Mimi ……...ambaye ni mzazi / mlezi wa mwanafunzi ……(jina la mwanafunzi) nimesoma maelekezo na maagizo kwa mwanafunzi na ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katuka kumlea kijana katika mwenendo na maadili mema. Aidha naahidi kutimiza mahitaji yake yote kwa wakati bila kumletea mwanafunzi katika swala zima la taaluma.

Tarehe:…… **Sahihi mzazi/mlezi:……**